

## MASIKU KUMI YA MWANZO NDANI YA MWEZI WA DHULHIJJAH

عن ابن عباس - رضي الله عنهمَا - عن النبي - ﷺ - قال: (ما من أيام العمل الصالح فيهن أحب إلى الله منه في هذه الأيام العشر، قالوا: ولا الجهاد في سبيل الله، إلا رجل خرج بنفسه وماله ولم يرجع من ذلك بشيء) أخرجه البخاري وأبو داود والترمذى وابن ماجة وأحمد

الحديث دليل على فضل أيام عشر ذي الحجة على غيرها من أيام السنة، لأن النبي - ﷺ - شهد بأنها أفضل أيام الدنيا، وأنه حث على العمل الصالح فيها. وفيه دليل على أن كل عمل صالح في هذه الأيام فهو أحب إلى الله تعالى منه في غيرها، وهذا يدل على فضل العمل الصالح فيها وكثرة ثوابه، وأن جميع الأعمال الصالحة تضاعف في العشر من غير استثناء شيء منها.

وعن ابن عباس - رضي الله عنهمَا - عن النبي - ﷺ - قال: (ما من عمل أركى عند الله عز وجل، ولا أعظم أجراً من خير يعمله في عشر الأضحى) قيل: ولا الجهاد في سبيل الله؟ قال: (ولا الجهاد في سبيل الله - عز وجل - إلا رجل خرج بنفسه وماله فلم يرجع من ذلك بشيء) رواه الدارمي بإسناد حسن وإن إدراك هذه العشر نعمة عظيمة من نعم الله تعالى على عبده، لأنه يدرك موسمًا من مواسم الطاعة التي تكون عوناً لل المسلم - بتوفيق الله - على تحصيل الثواب واغتنام الأجر، فعل المسلم أن يستشعر هذه النعمة، ويستحضر عظم أجر العمل فيها، ويعتزم الأوقات، وأن يُظهر لهذه العشر مزية على غيرها، بمزيد الطاعة، وهذا شأن سلف هذه الأمة، كما قال أبو عثمان الهمي - رحمه الله

وفي العشر أعمال فاضلة وطاعة كثيرة، ومن ذلك: 1 الإكثار من نوافل الصلاة، والصدقة، وسائر الأعمال الصالحة، كبر الوالدين، وصلة الأرحام، والتوبية النصوح، وحسن الإنابة، ونحو ذلك. 2 الإكثار من ذكر الله تعالى، وتكبيره، وتلاوة كتابه. 3 - الصيام، فإن صيام تسع ذي الحجة وإن لم يثبت فيها دليل بخصوصه في العشر، لكنه من أفضل الأعمال الصالحة التي حث عليها النبي - ﷺ -، فيكون استحباب صومها مستفاداً من عموم الأدلة. 4 - الحج والعمرة، وهما من أفضل الأعمال، كما سيأتي إن شاء الله. 5 الحرص على الأضحية وعدم التهاون فيها، لعظم أجرها عند الله تعالى.

اللهم أیقظنا من رقدات الغفلة، ووقفنا للاستعداد قبل النقلة، وارزقنا اغتنام الزمان وقت المهلة، وأطعمنا الاستفادة من مواسم الخيرات، وصلّى الله وسلم على نبينا محمد ...

Kutoka kwa Abdullaah Ibnu Abbaas Allah amridhie , amesimulia kutoka kwa Mtume ﷺ amesema [[ Hakuna masiku yoyote ambayo matendo mema yanapendwa zaidi na Allah kuliko matendo mema ya masiku haya kumi. Wakauliza maswahaba 'Wala tendo la jihadi katika njia ya Allah?' Akajibu "Wala tendo la jihadi katika njia ya Allah, isipokuwa mtu ambaye ametoka na nafsi yake na mali yake kwenda katika jihadi , na wala hakiku-rejea chochote katika hivyo ]] Bukhari, Ahmad, Tirmidhiy na Ibnu Maajah.

**H**adithi hii ni dalili kuhusu ubora wa masiku kumi ya mwanzo katika mwezi wa Dhulhijjah kuliko masiku mengine katika mwaka. Kwa sababu Mtume ﷺ ameshuhudia kwamba masiku hayo ni bora kuliko masiku yote ya duniani, na amehamasisha kutenda matendo mema ndani yake. Na ndani ya hadithi hiyo pia kuna dalili ya kwamba kila tendo jema ndani ya masiku hayo hupendwa zaidi na Allah Mtukufu kuliko tendo jema lolote katika masiku mengine. Na hii inajulisha juu ya ubora mkubwa wa matendo mema ndani yake na wingi wa malipo yake na kwamba matendo yote mema yatendwayo ndani ya masiku hayo huongezwa malipo yake pasina kubagua tendo jema lolote.

Kutoka kwa Abdullaah Ibnu Abbaas Allah amridhie , amesimulia kutoka kwa Mtume ﷺ amesema [[ Hakuna matendo yoyote yaliyo bora zaidi mbele ya Allah na yenye malipo makubwa zaidi kuliko matendo mema ayatendayo mtu ndani ya masiku kumi ya mwanzo katika mwezi wa Dhulhijjah Wakauliza maswahaba 'Wala tendo la jihadi katika njia ya Allah?' Akajibu "Wala tendo la jihadi katika njia ya Allah, isipokuwa mtu ambaye ametoka na nafsi yake na mali yake kwenda katika jihadi , na wala hakiku-rejea chochote katika hivyo ]] Addaarimiyy.

**H**akika kuyapata masiku haya kumi ya mwanzo katika mwezi wa Dhulhijjah ni neema kubwa sana mionganoni mwa neema za Allah juu ya mja wake, kwa sababu anakuwa kaupata msimu mionganoni mwa misimu (ya kipekee) ya kumtii Allah ambayo inakuwa ni msaada kwa muislamu – kwa uwezeshaji wa Allah– unakuwa ni msaada kwa muislamu katika kupata thawabu kemkem na kupata malipo mengi. Ni wajibu juu ya kila muislamu atambue neema hii na ahudhurishe moyoni mwake ukubwa wa malipo yaliyomo ndani ya masiku haya na azitumie vema nyakati na aonyeshe upekee na utofauti wa masiku haya kumi dhidi ya masiku mengine; kwa kuzidisha utendaji wa kumtii Allah, na hiyo ndio hali ya wema waliotangulia wa umma huu; kama alivyosema Abuu Uthmaan Annahdiy, Allah amrehemu {{Wema waliotangulia walikuwa wanazitukiza siku kumi za aina tatu; **Siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhan**, na **Siku kumi za mwanzo za mwezi wa Dhulhijjah** na **Siku kumi za mwanzo za mwezi wa Muharram.** }}

Na ndani ya siku kumi za mwanzo wa mwezi wa Dhulhijjah kuna matendo mengi mno yaliyobora (kufanywa) na ya kumtii Allah , mionganoni mwa hayo ni haya yafuatayo:

- 1) **Kuzidisha swala za sunna na sadaka na matendo mema mengineyo**, kama vile kuwafanya wema wazazi wawili na kuunga ndugu wa karibu, na kufanya toba ya kweli, na

kujisogea kwa Allah kwa wema, na mfano wa hayo.

- (2) **Kuzidisha kumtaja Allah Mtukufu, na kumtukiza na kusoma Qur'an.**
- (3) **Kufunga swaumu.** Hakika swaumu ya masiku tisa ya mwanzo katika mwezi wa Dhulhijjah, japokuwa haikuthibitika hadithi maalumu kwa ajili ya swaumu hiyo; lakini swaumu ni mojawapo ya matendo mema yaliyo bora mno ambayo Mtume ﷺ ameyasisitiza sana, hivyo kupendelewa swaumu ndani ya masiku haya tisa ni kutokana na ujumla wa dalili za ubora wa swaumu za sunna.
- (4) **Ibada ya Hija na Umra**, nazo ni mionganoni mwa ibada bora zaidi.
- (5) **Kupupia katika ibada ya kuchinja na kutoizembea**, kwa sababu ya ukubwa wa malipo yake mbele ya Allah Mtukufu.



we Allah tunakuomba utuzindue katika usingizi wa kujisahau na utuwezeshe tufanye maandalizi ya akhera kabla ya kutoka duniani na uturuzuku msaada wako wa kutumia muda na nyakati za uhai wetu na utupe uzindushi wa kuitumia misimu ya kheri.

وَصَلَى اللَّهُ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ وَصَحْبِهِ وَسَلَّمَ

Mkusanyaji na Mkalimani: Ummati Abdallah, Abuu Muhammad

المصدر: أحاديث عشر ذي الحجة وأيام التشريق أحكام وآداب، عبدالله بن صالح الفوزان